



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

SENSA YA WATU NA MAKAZI YA MWAKA 2022 MATOKEO YA MWANZO



OKTOBA 2022



Nukuu:

Wizara ya Fedha na Mipango, Ofisi ya Taifa ya Takwimu – Tanzania na Ofisi ya Rais - Fedha na Mipango, Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali Zanzibar. Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022: Matokeo ya Mwanzo. Dodoma, Tanzania. Oktoba 2022



Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

Matokeo ya Mwanzo ya
Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022

Wizara ya Fedha na Mipango
Ofisi ya Taifa ya Takwimu
Tanzania

na

Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango
Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali
Zanzibar

Oktoba 2022



THE WORLD BANK

YALIYOMO

DIBAJI	ii
SHUKRANI	iv
MUHTASARI WA Viashiria Muhimu kwa Tanzania, Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar	vi
UtanguliZi	1
Mgawanyo wa Watu	3
SENSA YA Majengo	13
ANWANI ZA MAKAZI	18
Huduma za Jamii	21
MGAWANYO WA IDADI YA WATU, IDADI YA MAJENGO, NA IDADI YA HUDUMA ZA KIJAMII KWA MKOA	27
KIAMBATISHO A: DODOSO LA SENSA	90



Serikali ya Awamu ya Sita, chini ya uongozi wangu imetimiza wajibu wake wa kufanya Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022 kama ilivyofanyika katika Awamu nyingine Tano zilizopita ambapo Sensa hizo zilifanyika katika miaka ya 1967, 1978, 1988, 2002 na 2012. Sensa hii imefanyika kwa mujibu wa Sheria ya Takwimu SURA 351 ambayo inaelekeza Serikali kufanya Sensa ya Watu na Makazi kila baada ya miaka kumi. Halikadhalika, Sensa imefanyika kukidhi matakwa ya kimataifa ambapo Umoja wa Mataifa unazitaka nchi kufanya Sensa ya Watu na Makazi angalau mara moja ndani ya miaka kumi. Sensa ya Mwaka 2022 imefanyika katika kipindi cha utekelezaji wa Mpango Mkakati wa Umoja wa Mataifa wa kufanya Sensa katika miaka ya 2020 ambao ulianza mwaka 2015 na utashia mwaka 2024.

Matokeo ya Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022 ni kwa ajili ya mipango jumuishi na maendeleo endelevu ya nchi na yataongeza uwazi katika kugawa rasilimali zilizopo kuendana na uwiano wa idadi ya watu katika ngazi zote za utawala. Halikadhalika matokeo yatumika na Serikali na wadau wengine katika kufuatilia na kutathmini mipango mbalimbali ya kitaifa na kimataifa ikijumuisa Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025 na Dira ya Zanzibar 2050, Mpango wa Tatu wa Taifa wa Maendeleo wa Mwaka 2021/22 - 2025/26 na Mpango wa Maendeleo wa Zanzibar (2021/22 - 2025/26), Dira ya Maendeleo ya Jumuiya ya Afrika Mashariki 2050 na Ajenda ya Maendeleo ya Afrika 2063. Taarifa hizi zitaipima Tanzania katika hatua iliyofikia kwenye utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu; Mpango ambao unalenga kuleta usawa na kutokomeza umaskini wa aina zote ukiwemo umaskini uliokithiri ifikapo mwaka 2030 kwa kuhakikisha kuwa hakuna mtu anayeachwa nyuma.

Chapisho la Matokeo ya mwanzo ni la kwanza katika mtiririko wa machapisho yaliyopangwa kutolewa kutokana na Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022. Dhumuni kuu la kuandaa chapisho hili ni kutangaza jumla ya idadi ya watu waliohesabiwa nchini kwa jinsi na kwa mikoa. Taarifa hii ni muhimu kwa vile itajulisha umma hali halisi ya idadi ya watu nchini, Tanzania Bara na Zanzibar na kwa kila mkoa. Aidha, mwenendo wa ongezeko la watu kutoka Sensa ya mwaka 1967

mpaka 2022 umeainishwa. Chapisho hili litatoa pia jumla ya majengo yote nchini, aina ya majengo na majengo yenye anwani za makazi na huduma za jamii.

Nitumie nafasi hii pia kutoa shukrani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Dkt. Philip Isidor Mpango - Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi - Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb.) - Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na mwenyekiti wa Kamati Kuu ya Taifa ya Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022, Mheshimiwa Othman Masoud Othman - Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, pamoja na Mheshimiwa Hemed Suleiman Abdulla (MBW) - Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar na mwenyekiti mwenza wa Kamati Kuu ya Taifa ya Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022 kwa uongozi na usimamizi madhubuti wa mchakato mzima wa utekelezaji wa zoezi la Sensa pamoja na majukumu mengine ya kitaifa.

Kwa namna ya kipekee ninawashukuru Mheshimiwa Anne Semamba Makinda - Kamisaa wa Sensa Tanzania Bara na Spika Mstaafu wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mheshimiwa Balazi Mohamed Haji Hamza - Kamisaa wa Sensa Tanzania Zanzibar kwa namna ambavyo wameongoza na kusimamia vyema kazi ya kuelimisha na kuhamasisha wananchi kushiriki katika zoezi la sensa na hatimaye kufanikisha zoezi zima la Sensa kwa wakati na kwa ubora wa hali ya juu.

Samia Suluhu Hassan

RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

SHUKRANI



Napenda kutoa shukrani za dhiti kwa wenyeviti wenza wa Kamati ya Taifa ya Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022 Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb.) - Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar Mheshimiwa Hemed Suleiman Abdulla (MBW) kwa miongozo na maelekezo yao yaliyofanikisha Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022. Aidha, ufanikishaji wa zoezi hili ni kutokana na ushirikiano mkubwa wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, wizara, idara na taasisi za Serikali kwa pande zote mbili za Muungano, wadau wa maendeleo, pamoja na wataalam mbalimbali ambao utaalamu wao umewezesha kukamilika kwa zoezi la Sensa.

Nawashukuru pia wajumbe wote wa Kamati Kuu ya Taifa ya Sensa, Kamati ya Taifa ya Ushauri ya Sensa, Kamati ya Ushauri wa Kiufundi, Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, Zanzibar. Kwa upande mwingine natoa shukrani za dhiti kwa Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya, Madiwani, Waratibu wa Sensa Taifa, Waratibu wa Sensa wa mikoa na wilaya, viongozi wa kata/shehia, mitaa na vitongoji, wasimamizi, makarani wa Sensa na wakuu wa kaya kwa kutimiza majukumu yao ipasavyo na kufanikisha zoezi la Sensa katika maeneo yao ya utawala.

Shukrani za kipekee ni kwa washirika wa maendeleo ikiwemo UNFPA, UN-Women, UNICEF, USAID, IOM, FCDO, Benki ya Dunia, Ofisi ya Sensa ya Marekani (US Census Bureau), Ubalozi wa Korea Kusini Nchini Tanzania na washirika wengine wa maendeleo kwa kutoa msaada wa vifaa, utaalamu, mafunzo na fedha katika kufanikisha zoezi la Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022. Tunawashukuru pia viongozi wa dini, viongozi wa kimila, viongozi wa vyama vya siasa, viongozi wa mashirika mbalimbali yasiyo ya Serikali, vyombo vya Habari na wananchi wote kwa ujumla kwa ushiriki na michango yao katika kufanikisha zoezi la Sensa.

Kwa namna ya pekee, nawashukuru Mheshimiwa Anne Semamba Makinda - Kamisaa wa Sensa Tanzania Bara na Spika mstaafu wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mheshimiwa Balozi Mohammed Haji Hamza - Kamisaa wa

Sensa Zanzibar; Mwenyekiti wa Bodi ya Usimamizi ya Ofisi ya Taifa ya Takwimu Dkt. Amina Msengwa; na Mwenyekiti wa Bodi ya Takwimu, Zanzibar Mheshimiwa Balozi Amina Salum Ali kwa uongozi na maelekezo sahihi katika kipindi chote cha utekelezaji wa zoezi la Sensa. Shukrani za pekee kwa menejimenti na watumishi wote wa Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS) ikiongozwa na Dkt. Albina Chuwa; Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali, Zanzibar (OCGS) Bw. Salum Kasim Ali; watumishi wa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi; Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari; na watumishi wengine wa Serikali kwa kufanya kazi kwa weledi wa hali ya juu na bila kuchoka katika kuhakikisha Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022 inafanikiwa kwa mafanikio makubwa.

Dkt. Hussein Ali Mwinyi

RAIS WA ZANZIBAR NA MWENYEKITI WA BARAZA LA MAPINDUZI

**MUHTASARI WA VIASHIRIA MUHIMU KWA TANZANIA,
TANZANIA BARA NA TANZANIA ZANZIBAR**

Viashiria	Tanzania		Tanzania Bara		Tanzania Zanzibar	
	Idadi	%	Idadi	%	Idadi	%
IDADI YA WATU						
Jumla	61,741,120	100.0	59,851,347	100.0	1,889,773	100.0
Wanaume	30,053,130	48.7	29,137,638	48.7	915,492	48.4
Wanawake	31,687,990	51.3	30,713,709	51.3	974,281	51.6
Uwiano Kijinsi		95		95		94
Kasi ya Ongezeko la Watu (2012 - 2022)		3.2		3.2		3.7
MAJENGO						
Jumla	14,348,372	100.0	13,907,951	100.0	440,421	100.0
Majengo ya Ghorofa	68,724	0.5	61,258	0.4	7,466	1.7
Yasiyo ya Ghorofa	13,540,363	94.4	13,152,298	94.6	388,065	88.1
Yanayoendelea na ujenzi	739,285	5.1	694,395	5.0	44,890	10.2
ANWANI ZA MAKAZI						
Majengo yenye Anwani za Makazi	10,751,123	74.9	10,406,722	74.8	344,401	78.2
Majengo yasiyo na Anwani za Makazi	3,597,249	25.1	3,501,229	25.2	96,020	21.8
VITUO VYA KUTOLEA HUDUMA ZA AFYA						
Zahanati	7,965	78.8	7,680	78.6	285	85.1
Vituo vya Afya	1,466	14.5	1,430	14.6	36	10.7
Hospitali	676	6.7	662	6.8	14	4.2
HUDUMA ZA ELIMU						
Shule za Msingi	19,769	77.1	19,266	77.5	503	65.5
Shule za Sekondari	5,857	22.9	5,592	22.5	265	34.5

UTANGULIZI

Sensa ya Watu na Makazi ni utaratibu wa kukusanya, kuchakata, kuchambua, kutathmini, kuchapisha, kusambaza na kutunza takwimu za kidemografia, kiuchumi na mazingira wanayoishi katika nchi kwa kipindi maalum. Utaratibu huu huwezesha kupatikana kwa taarifa za msingi za kitakwimu kama idadi ya watu wote kwenye nchi kwa umri, jinsi, hali ya ulemavu, hali ya elimu, shughuli za kiuchumi, hali ya makazi, vizazi, vifo na nyingine kama zilivyoainishwa katika Dodoso la Sensa (**Angalia Kiambatisho A**).

Dhumuni kuu la kufanya Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022 ni kupata viashiria vya msingi vya watu na makazi ambavyo vitawezesha katika kutunga sera, kupanga, kufuatilia mipango ya maendeleo ya kimkakati inayolenga kukuza ustawi wa nchi na wananchi. Aidha, matokeo ya Sensa yataiwezesha Serikali na wadau wengine kufuatilia na kutathmini malengo yaliyofikiwa katika utekelezaji wa mipango ya maendeleo iliyokusudiwa kwa lengo la kukuza uchumi na ustawi wa jamiin a hatimae kupunguza umaskini.

Utofauti wa Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022 na sensa zilizopita umepelekea kuwa na ubora wa hali ya juu wa takwimu za sensa. Sensa hii imetumia teknolojia ya kidigitali katika utekelezaji wake kuanzia kwenye zoezi la utengaji wa maeneo ya kijiografia ya kuhesabia watu katika ngazi za shehia, mitaa na vitongoji, hadi kwenye zoezi la kuhesabu watu. Matumizi ya vishikwambi (tablets) katika hatua zote za utekelezaji kumesaidia katika kupunguza gharama za uendeshaji, usomaji wa majira nukta katika kaya, majengo, ukusanyaji Taarifa kutoka katika huduma zote za jamii na katika zoezi la kuhesabu watu na hii imechangia kwa kiasi kikubwa katika kuboresha taarifa zilizokusanywa. Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022 imekusanya taarifa nyingi zaidi ambapo Dodoso Kuu lilikuwa na maswali 100 ikilinganishwa na sensa ya 2012 ambayo ilikuwa na maswali 64. Hali hii imesababishwa na mabadiliko makubwa ya kiuchumi duniani pamoja na kuongezeka zaidi kwa matumizi ya teknolojia kulikosababisha uwepo wa mahitaji makubwa ya takwimu nchini.

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ilifanya maamuzi ya utekelezaji wa Sensa ya Majengo na Sensa ya Anwani za Makazi kwa kutumia mfumo wa utekelezaji wa Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022 kwa lengo la kuongeza

ufanisi na kuipunguzia Serikali gharama ya kufanya mazoezi matatu makubwa katika vipindi tofauti. Taarifa za majengo na anwani za makazi ni kielelezo muhimu sana kwa Taifa na kwa mwananchi mmoja mmoja kwa ajili ya makazi na shughuli nyingine muhimu za maendeleo. Sensa ya Majengo na Anwani za Makazi ni zoezi ambalo limefanyika kwa mara ya kwanza Nchini tangu kuasisiwa kwa muungano wa Tanganyika na Zanzibar mwaka 1964. Taarifa za majengo zilikuwa zinakusanywa katika tafiti za kitaifa zilizokuwa zinafanyika kila baada ya miaka mitano kwa ajili ya kuboresha sera ya mipango Nchi.


Taarifa za majengo yote Nchini na anwani za makazi zitaiwezesha Serikali katika kuandaa sera, sheria, kanuni za mipango miji na programu mbalimbali za maendeleo katika Taifa. Halikadhalika, taarifa za majengo na anwani za makazi za mwaka 2022 zitatumika katika kujitathmini kwa miaka ijayo katika uandaaji wa taarifa za utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDG) na Agenda 2030 ya Shirika la Umoja wa Mataifa la Makazi (*UN-Habitat*).

Hata hivyo, uwekaji wa anwani za makazi ni endelevu, hivyo Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar zitaendelea na zoezi la uwekaji wa anwani za makazi na ukusanyaji wa taarifa za majengo yote yanayotarajiwa kujengwa nchini, ili kuweza kuhuisha kanzidata za majengo na anwani za makazi.

MGAWANYO WA WATU


Matokeo ya Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022 yanaonesha kuwa, idadi ya watu nchini imeongezeka kutoka 44,928,923 waliohesabiwa mwaka 2012 hadi kufikia watu 61,741,120 kwa mwaka 2022, sawa na wastani wa ongezeko la idadi ya watu kwa mwaka (the annual intercensal population growth rate) la asilimia 3.2. Kwa Tanzania Bara, idadi ya watu imeongezeka kutoka 43,625,354 mwaka 2012 hadi watu 59,851,347 mwaka 2022 wakati kwa Tanzania Zanzibar idadi ya watu imeongezeka kutoka 1,303,569 mwaka 2012 hadi watu 1,889,773 mwaka 2022 (Angalia Kielelezo Na. 1)

Kielelezo Na. 1: Ongezeko la Idadi ya Watu (kwa Milioni) Tanzania, Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2012 na 2022




Kati ya watu 61,741,120 waliohesabiwa mwaka 2022 katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, wanaume ni 30,053,130 sawa na asilimia 49 ya watu wote nchini na wanawake ni 31,687,990 sawa na asilimia 51. Kwa Tanzania Bara, kati ya watu 59,851,347 waliohesabiwa, wanaume ni 29,137,638 sawa na asilimia 49 ya watu wote Tanzania Bara na wanawake ni 30,713,709 sawa na asilimia 51. Kwa Tanzania Zanzibar, kati ya watu 1,889,773 waliohesabiwa, wanaume ni 915,492 sawa na asilimia 48 ya watu wote Tanzania Zanzibar na wanawake ni 974,281 sawa na asilimia 52 (Angalia Kielelezo Na. 2 na 3).

Kielelezo Na. 2: Idadi ya Watu kwa Jinsi: Tanzania, Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar




Kielelezo Na. 3: Mgawanyo wa Watu kwa Jinsi



MWENENDO WA ONGEZEKO LA IDADI YA WATU TANZANIA, KUENZIA MWAKA 1967 HADI 2022

Kielelezo Na. 4 kinaonesha kwamba idadi ya watu nchini imeongezeka **MARA TANO** kutoka mwaka 1967. Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022 imeonesha kuwa idadi ya watu imeongezeka kutoka 12,313,469 mwaka 1967 hadi kufikia watu 61,741,120 mwaka 2022.

Kielelezo Na. 4: Ongezeko la Idadi ya Watu, Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 1967 - 2022




IDADI YA WATU KWA MIKOA


Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kiutawala ina jumla ya mikoa 31. Mikoa 26 iko Tanzania Bara na mikoa mitano iko Tanzania Zanzibar. Matokeo yanaonesha kuwa mkoa wenye watu wengi zaidi ya mikoa mingine ni Dar es Salaam, ukiwa na idadi ya watu 5,383,728 ambayo ni sawa na asilimia 8.7 ya watu wote nchini. Mikoa ambayo ina watu zaidi ya milioni tatu ni pamoja na Mwanza (3,699,872), Tabora (3,391,679), Morogoro (3,197,104) na Dodoma (3,085,625).

Kwa Tanzania Bara mkoa wenye idadi ya watu chini ya milioni moja ni Njombe, ambao una watu 889,946. Aidha, mikoa yote ya Tanzania Zanzibar ina watu chini ya milioni moja, (Angalia Ramani Na. 1).

Ramani Na. 1: Mgawanyo wa Idadi ya Watu kwa Mkoa



Kielelezo Na. 5: Mgawanyo wa Idadi ya Watu kwa Mkoa (katika Milioni) kwa Senza ya Watu na Makazi ya Mwaka 2012 na 2022




Jedwali Na. 1: Idadi ya Watu kwa Mikoa na Jinsi

Eneo	Jumla	Wanaume	Wanawake
Tanzania	61,741,120	30,053,130	31,687,990
Tanzania Bara	59,851,347	29,137,638	30,713,709
Dodoma	3,085,625	1,512,760	1,572,865
Arusha	2,356,255	1,125,616	1,230,639
Kilimanjaro	1,861,934	907,636	954,298
Tanga	2,615,597	1,275,665	1,339,932
Morogoro	3,197,104	1,579,869	1,617,235
Pwani	2,024,947	998,616	1,026,331
Dar es Salaam	5,383,728	2,600,018	2,783,710
Lindi	1,194,028	582,120	611,908
Mtwara	1,634,947	776,782	858,165
Ruvuma	1,848,794	902,298	946,496
Iringa	1,192,728	574,313	618,415
Mbeya	2,343,754	1,123,828	1,219,926
Singida	2,008,058	995,703	1,012,355
Tabora	3,391,679	1,661,171	1,730,508
Rukwa	1,540,519	743,119	797,400
Kigoma	2,470,967	1,186,833	1,284,134
Shinyanga	2,241,299	1,102,879	1,138,420
Kagera	2,989,299	1,459,280	1,530,019
Mwanza	3,699,872	1,802,183	1,897,689
Mara	2,372,015	1,139,511	1,232,504
Manyara	1,892,502	954,879	937,623
Njombe	889,946	420,533	469,413
Katavi	1,152,958	569,902	583,056
Simiyu	2,140,497	1,034,681	1,105,816
Geita	2,977,608	1,463,764	1,513,844
Songwe	1,344,687	643,679	701,008
Tanzania Zanzibar	1,889,773	915,492	974,281
Kaskazini Unguja	257,290	126,341	130,949
Kusini Unguja	195,873	98,367	97,506
Mjini Magharibi	893,169	427,927	465,242
Kaskazini Pemba	272,091	131,484	140,607
Kusini Pemba	271,350	131,373	139,977

UWIANO WA KIJINSI

Uwiano wa idadi ya watu kijinsi kwa Tanzania na Tanzania Bara ni wanaume 95 kwa kila wanawake 100, wakati kwa upande wa Tanzania Zanzibar ni wanaume 94 kwa kila wanawake 100. Mkoa wa Manyara una idadi kubwa ya wanaume kuliko wanawake ukilinganisha na mikoa mingine ambapo kwa kila wanawake 100, kuna wanaume 102. Mkoa wa Njombe umeonekana kuwa na uwiano mdogo zaidi wa kijinsi wa wanaume 90 kwa kila wanawake 100 ukilinganishwa na mikoa mingine (Angalia Kielelezo Na. 6).


Kielelezo Na. 6: Uwiano wa Watu Kijinsi kwa Mkoa



WASTANI WA KASI YA ONGEZECO LA IDADI YA WATU KWA MWAKA


Wastani wa kasi ya ongezeko la idadi ya watu Tanzania kwa mwaka imeongezeka kutoka asilimia 2.7 mwaka 2012 hadi asilimia 3.2 mwaka 2022. Kasi ya ongezeko kwa Tanzania Bara ni sawa na ile ya Kitaifa. Kwa Tanzania Zanzibar wastani wa kasi ya ongezeko la idadi ya watu kwa mwaka iliongezeka kutoka asilimia 2.8 mwaka 2012 hadi asilimia 3.7 mwaka 2022 (Angalia Kielelezo Na. 7).

Kielelezo Na. 7: Wastani wa Kasi ya Ongezeko la Idadi ya Watu kwa Sensa za Watu na Makazi 1988–2002, 2002–2012, na 2012–2022



Idadi ya watu Tanzania na Tanzania Bara kwa mwaka 2022 imekuwa ikiongezeka kwa wastani wa asilimia 3.2 na Tanzania Zanzibar imekuwa ikiongezeka kwa wastani wa asilimia 3.7.

Kielelezo Na. 8: Kasi ya Ongezeko la Idadi ya Watu kwa Mkoa



Kasi ya ongezeko la idadi ya watu kwa mkoa wa Dar es Salaam imepungua kutoka asilimia 5.6 kwa Mwaka 2012 hadi asilimia 2.1 kwa Mwaka 2022.

Kasi ya ongezeko la idadi ya watu kwa mkoa wa Kilimanjaro imepungua kutoka asilimia 1.8 mwaka 2012 hadi asilimia 1.3 mwaka 2022.

SENSA YA MAJENGO

Sambamba na Sena ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022, Serikali pia imefanya Sena ya Majengo nchini.

IDADI YA MAJENGO

Matokeo ya Sena ya Majengo ya Mwaka 2022 yanaonesha kuwa, idadi ya majengo yote nchini ni 14,348,372, ambapo majengo 13,907,951 yapo Tanzania Bara na Majengo 440,421 yapo Tanzania Zanzibar.

AINA ZA MAJENGO

Kati ya majengo 14,348,372 yaliyopo nchini, majengo 68,724 ni ya ghorofa, majengo 13,540,363 sio ya ghorofa, na majengo 739,285 yapo katika hatua ya ujenzi. Majengo ya ghorofa yaliyoko Tanzania Bara ni 61,258 na yaliyopo Tanzania Zanzibar ni 7,466 (Angalia Jedwali Na. 2).

Jedwali Na. 2: Idadi ya Majengo kwa Aina ya Jengo na Maeneo

Eneo	Jumla	Aina ya Jengo		
		Ghorofa	Yasiyo ya Ghorofa	Yanayoendelea na ujenzi
Tanzania	14,348,372	68,724	13,540,363	739,285
Tanzania Bara	13,907,951	61,258	13,152,298	694,395
Tanzania Zanzibar	440,421	7,466	388,065	44,890

IDADI YA MAJENGO KWA AINA NA MIKOA


Matokeo ya Sensa ya Majengo ya Mwaka 2022 yanaonesha kuwa mkoa wenye majengo mengi zaidi mingine ni Dar es Salaam (majengo 913,707) ukifuatiwa na Mwanza (majengo 868,430) na Dodoma (majengo 836,909). Mkoa wa Dar es Salaam pia una majengo mengi zaidi ya ghorofa (majengo 32,219) ambayo ni sawa na asilimia 47 ya majengo yote ya ghorofa nchini, (Angalia Jedwali Na. 3).

Jedwali Na. 3: Idadi ya Majengo kwa Aina na Mkoa

Eneo	Jumla	Ghorofa	Yasiyo ya Ghorofa	Yanaendelea na ujenzi
Tanzania	14,348,372	68,724	13,540,363	739,285
Tanzania Bara	13,907,951	61,258	13,152,298	694,395
Dodoma	836,909	1,461	794,209	41,239
Arusha	553,702	7,180	515,560	30,962
Kilimanjaro	515,091	3,540	486,916	24,635
Tanga	676,397	4,282	638,604	33,511
Morogoro	762,454	1,331	724,320	36,803
Pwani	504,979	1,885	468,005	35,089
Dar es Salaam	913,707	32,219	827,644	53,844
Lindi	341,398	327	326,065	15,006
Mtwara	511,336	507	488,078	22,751
Ruvuma	448,328	408	434,989	12,931
Iringa	357,777	529	339,561	17,687
Mbeya	623,054	1,073	592,896	29,085
Singida	463,353	290	440,541	22,522
Tabora	680,103	400	648,178	31,525
Rukwa	302,368	173	290,707	11,488
Kigoma	458,567	318	444,481	13,768
Shinyanga	421,743	358	398,581	22,804
Kagera	716,458	701	684,987	30,770
Mwanza	868,430	2,481	801,826	64,123
Mara	636,185	510	595,721	39,954
Manyara	430,323	318	406,054	23,951
Njombe	279,349	322	270,529	8,498
Katavi	189,349	70	180,146	9,133
Simiyu	430,378	138	414,145	16,095
Geita	624,100	263	587,719	36,118
Songwe	362,113	174	351,836	10,103

Eneo	Jumla	Ghorofa	Yasiyo ya Ghorofa	Yanaendelea na ujenzi
Tanzania Zanzibar	440,421	7,466	388,065	44,890
Kaskazini Unguja	74,764	466	66,676	7,622
Kusini Unguja	64,453	850	54,117	9,486
Mjini Magharibi	177,450	5,453	154,249	17,748
Kaskazini Pemba	63,490	222	58,280	4,988
Kusini Pemba	60,264	475	54,743	5,046

Kielelezo Na. 9: Idadi ya Majengo kwa Mkoa (“00,000”)



Ramani Na. 2: Idadi ya Majengo kwa Mikoa



ANWANI ZA MAKAZI

MAJENGO YENYE ANWANI ZA MAKAZI

Kati ya majengo 14,348,372 yaliyohesabiwa wakati wa sensa, majengo yenye anwani za makazi ni 10,751,123 sawa na asilimia 74.9 ya majengo yote nchini; wakati majengo 3,597,249 sawa na asilimia 25.1 hayana anwani za makazi. Kwa Tanzania Bara, majengo 10,406,722 sawa na asilimia 74.8 ya majengo yote Tanzania Bara yana anwani za makazi, wakati kwa Tanzania Zanzibar, majengo 440,421 sawa na asilimia 78.2 ya majengo yote Tanzania Zanzibar yana anwani za makazi (Angalia Jedwali Na. 4).

Jedwali Na. 4: Idadi ya Majengo yenye Anwani za Makazi

Eneo	Idadi ya Majengo		
	Jumla	Majengo yenye Anwani ya Makazi	Majengo yasiyo na Anwani za Makazi
Tanzania	14,348,372	10,751,123	3,597,249
Tanzania Bara	13,907,951	10,406,722	3,501,229
Tanzania Zanzibar	440,421	344,401	96,020


MAJENGO YENYE ANWANI ZA MAKAZI KWA MIKOA

Matokeo ya Sensa yanaonesha kuwa mkoa ambao majengo yake mengi yana anwani za makazi ni **Kaskazini Pemba (asilimia 89.9)** na mikoa mingine ambayo majengo yake zaidi ya asilimia 80 yana anwani za makazi ni Mtwara (asilimia 88.2), Njombe (asilimia 87.7), Kusini Pemba (asilimia 84.5), Kagera (asilimia 83.5), Geita (asilimia 83.3), Ruvuma (asilimia 82.7), Simiyu (asilimia 81.9) na Lindi (asilimia 80.7). Mkoa wenye asilimia ndogo zaidi ya majengo yenye anwani za makazi ni Dodoma (asilimia 63.5) ikifuatiwa na Rukwa (asilimia 65.6) (Angalia Jedwali Na. 5).

Jedwali Na. 5: Idadi na Asilimia ya Majengo yenye Anwani za Makazi

Eneo	Idadi ya Anwani za Makazi			Asilimia
	Jumla	Yenye Anwani za makazi	Yasiyo na Anwani za Makazi	
Tanzania	14,348,372	10,751,123	3,597,249	74.9
Tanzania Bara	13,907,951	10,406,722	3,501,229	74.8
Dodoma	836,909	531,072	305,837	63.5
Arusha	553,702	410,498	143,204	74.1
Kilimanjaro	515,091	406,838	108,253	79.0
Tanga	676,397	482,127	194,270	71.3
Morogoro	762,454	536,095	226,359	70.3
Pwani	504,979	352,391	152,588	69.8
Dar es Salaam	913,707	638,673	275,034	69.9
Lindi	341,398	275,573	65,825	80.7
Mtwara	511,336	451,095	60,241	88.2
Ruvuma	448,328	370,620	77,708	82.7
Iringa	357,777	286,161	71,616	80.0
Mbeya	623,054	466,058	156,996	74.8
Singida	463,353	332,499	130,854	71.8
Tabora	680,103	482,033	198,070	70.9
Rukwa	302,368	198,424	103,944	65.6
Kigoma	458,567	353,519	105,048	77.1
Shinyanga	421,743	283,042	138,701	67.1
Kagera	716,458	598,332	118,126	83.5
Mwanza	868,430	637,231	231,199	73.4
Mara	636,185	490,774	145,411	77.1
Manyara	430,323	324,647	105,676	75.4
Njombe	279,349	244,920	34,429	87.7
Katavi	189,349	141,988	47,361	75.0
Simiyu	430,378	352,371	78,007	81.9
Geita	624,100	520,154	103,946	83.3
Songwe	362,113	239,587	122,526	66.2
Tanzania	440,421	344,401	96,020	78.2
Kaskazini	74,764	56,943	17,821	76.2
Kusini Uguja	64,453	49,243	15,210	76.4
Mjini Magharibi	177,450	130,218	47,232	73.4
Kaskazini Pemba	63,490	57,058	6,432	89.9
Kusini Pemba	60,264	50,939	9,325	84.5

Ramani Namba 3: Idadi ya Majengo yenye Anwani za Makazi kwa Mikoa



HUDUMA ZA JAMII

Siku mbili kabla ya kuanza kazi ya kuhesabu watu, makarani wa Sensa walihoji dodoso la jamii ili kupata Taarifa za huduma mbalimbali za jamii zilizopo kwenye Shehia, Mitaa na Vitongoji.

HUDUMA ZA AFYA

Matokeo yanaonesha kuwa Tanzania ina jumla ya hospitali 676, vituo vya afya 1,466 na zahanati 7,965. Kwa Tanzania Bara ina hospitali 662, vituo vya afya 1,430 na zahanati 7,680. Kwa upande wa Tanzania Zanzibar, matokeo ya Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022 yanaonesha kuwa kuna hospitali 14, vituo vya afya 36 na zahanati 285.

VITUO VYA KUTOLEA HUDUMA ZA AFYA KWA MIKOA

Jedwali Na. 6 linaonesha idadi ya vituo vya kutolea huduma za afya kwa mikoa yote 31 Tanzania. Mikoa iliyoonekana kuwa na hospitali zaidi ya 30 ni Dar es Salaam (76), Morogoro (44), Arusha (43), Mwanza (41), Mbeya (34) Kilimanjaro (33) na Mara (33) na mikoa yenye hospitali chini ya 10 ni Katavi (9), Mjini Magharibi (7), Kusini Pemba (3), Kaskazini Pemba (2), Kaskazini Unguja (1), na Kusini Unguja (1). Mikoa yenye vituo vya afya zaidi ya 60 ni pamoja na Dar es Salaam (154), Mwanza (103), Arusha (76), Morogoro (73), Mbeya (73), Dodoma (69), Kilimanjaro (66) na Tanga (64). Mikoa yenye zahanati zaidi ya 400 ni Dar es Salaam (454) Morogoro (415), Tanga (412) na Dodoma (402).

Jedwali Na. 6: Idadi ya Vituo vya Kutolea Huduma za Afya

Mkoa	Jumla	Zahanati	Vituo vya Afya	Hospitali
Tanzania	10,107	7,965	1,466	676
Tanzania Bara	9,772	7,680	1,430	662
Dodoma	497	402	69	26
Arusha	429	310	76	43
Kilimanjaro	461	362	66	33
Tanga	498	412	64	22
Morogoro	532	415	73	44
Pwani	444	365	57	22
Dar es Salaam	684	454	154	76
Lindi	303	253	34	16
Mtwara	312	257	38	17
Ruvuma	382	307	50	25
Iringa	349	283	47	19
Mbeya	443	336	73	34
Singida	282	229	30	23
Tabora	401	337	40	24
Rukwa	276	228	37	11
Kigoma	312	246	46	20
Shinyanga	311	250	46	15
Kagera	381	301	59	21
Mwanza	520	376	103	41
Mara	368	280	55	33
Manyara	290	236	38	16
Njombe	337	271	44	22
Katavi	134	100	25	9
Simiyu	289	243	28	18
Geita	290	227	43	20
Songwe	247	200	35	12
Tanzania Zanzibar	335	285	36	14
Kaskazini Unguja	47	41	5	1
Kusini Unguja	57	48	8	1
Mjini Magharibi	135	119	9	7
Kaskazini Pemba	47	39	6	2
Kusini Pemba	49	38	8	3

HUDUMA ZA ELIMU

Jedwali Na. 7 linaonesha idadi ya shule na kama ni ya msingi au sekondari. Matokeo yanaonesha kuwa Tanzania kuna shule za msingi 19,769 kati ya hizo, shule za msingi 19,266 ziko Tanzania Bara na 503 ziko Tanzania Zanzibar. Aidha matokeo yanaonesha zaidi kuwa kuna shule za sekondari 5,857, kati ya hizo shule 5,592 ziko Tanzania Bara na shule 265 ziko Tanzania Zanzibar.

IDADI YA SHULE KWA MIKOA

Kwa upande wa Tanzania Bara matokeo yanaonesha kuwa, mikoa yenye shule nyingi za sekondari ni Dar es Salaam (350), Kilimanjaro (349) na Mwanza (330) na mkoa wenye shule za sekondari chache zaidi ni Katavi (62) ukifuatiwa na Rukwa (97) na Songwe (130). Kwa upande wa Tanzania Zanzibar, mkoa wenye shule nyingi zaidi za sekondari ni Mjini Magharibi (84) na mkoa wenye shule za sekondari chache zaidi ni Kaskazini Unguja (39). Shule nyingi za msingi ziko mkoa wa Tanga (1,083), Mwanza (1,038) na Kagera (1,026) kwa Tanzania Bara wakati mikoa yenye shule za msingi chache zaidi ni Katavi (266), Rukwa (394) na Songwe (496). Kwa Tanzania Zanzibar, mkoa wa Mjini Magharibi una shule nyingi zaidi za msingi ikilinganishwa na mikoa mingine (Angalia Jedwali Na. 7).

Jedwali Na: 7: Idadi ya Shule kwa Mikoa na Aina

Mkoa	Jumla	Shule za Msingi	Shule za Sekondari
Tanzania	25,626	19,769	5,857
Tanzania Bara	24,858	19,266	5,592
Dodoma	1,060	827	233
Arusha	1,102	833	269
Kilimanjaro	1,348	999	349
Tanga	1,381	1,083	298
Morogoro	1,277	996	281
Pwani	932	713	219
Dar es Salaam	1,188	838	350
Lindi	663	530	133

Mkoa	Jumla	Shule za Msingi	Shule za Sekondari
Mtwara	857	692	165
Ruvuma	1,046	829	217
Iringa	735	544	191
Mbeya	1,073	807	266
Singida	797	630	167
Tabora	1,087	875	212
Rukwa	491	394	97
Kigoma	920	701	219
Shinyanga	843	671	172
Kagera	1,313	1,026	287
Mwanza	1,368	1,038	330
Mara	1,174	908	266
Manyara	875	692	183
Njombe	683	544	139
Katavi	328	266	62
Simiyu	759	592	167
Geita	932	742	190
Songwe	626	496	130
Tanzania Zanzibar	768	503	265
Kaskazini Unguja	106	67	39
Kusini Unguja	117	72	45
Mjini Magharibi	310	226	84
Kaskazini Pemba	113	67	46
Kusini Pemba	122	71	51

MAPENDEKEZO YA SERA

Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022 imefanyika sambamba na Sensa ya Majengo na Anwani za Makazi zoezi la kitaifa ambalo limefanyika kwa mara ya kwanza Nchini tangu kuasisiwa kwa muungano wa Tanganyika na Zanzibar mwaka 1964.

Wastani wa kasi ya ongezeko la idadi ya watu kutoka mwaka 2012 hadi 2022 ni asilimia 3.2, sawa na idadi ya watu 61,741,120 mwaka 2022, Tanzania Bara ikiwa na watu 59,851,347 na Tanzania Zanzibar 1,889,773. Kwa upande wa Sensa ya Majengo matokeo yamebainisha kuwa Tanzania ina majengo 14,348,372, kati ya hayo, asilimia 74.9 (10,751,123) yana anwani za makazi. Kwa upande wa huduma za afya, matokeo yameonesha Tanzania kuna vituo vya huduma za afya 10,107 na vituo vya huduma ya elimu 25,626 katika maeneo mbali mbali ya nchi.

Ujumbe wa Kisera

Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022 imeonesha kuongezeka kwa wastani wa kasi ya ongezeko la idadi ya watu kutoka asilimia 2.7 mwaka 2012 hadi asilimia 3.2 mwaka 2022. Kuongezeka kwa wastani wa kasi ya ongezeko la watu kutaathiri maeneo yafuatayo ya kisera:

- a. Uhitaji wa kuendelea kuongeza idadi ya vituo vya kutolea huduma za afya ili iendane na ongezeko la idadi ya watu kwa lengo la kuwa na jamii yenye afya njema inayoweza kushiriki katika shughuli za kiuchumi na kijamii kwa ufanisi;
- b. Uhitaji wa kuendelea kuongezeka idadi ya shule katika ngazi zote za kutolea huduma ya elimu kwa lengo la kujenga jamii iliyoelimika na ambayo itaweza kuajiriwa kwa urahisi ndani na nje ya nchi;
- c. Uhitaji wa kuendelea kuongeza uzalishaji wa mazao ya chakula na mazao, mifugo na mazao ya biashara wenye tija kwa lengo la kukidhi mahitaji ya chakula kwa wananchi wote na ziada ya kuuza nje ya nchi kwa ajili ya kujipatia fedha za kigeni;
- d. Uhitaji wa kujenga viwanda vya bidhaa mbalimbali ili kuziongezea thamani bidhaa zinazozalisha hapa nchini kwa ajili ya soko la ndani na nje ya nchi;
- e. Uhitaji wa kuendelea kujenga viwanda vya uzalishaji dawa na vifaa tiba ndani ya nchi kwa lengo la kupunguza matumizi ya fedha za kigeni katika uagizaji wa dawa na vifaa tiba;
- f. Uhitaji wa kuendelea kujenga viwanda vya uzalishaji wa bidhaa za ujenzi hapa nchini kwa lengo la kupunguza gharama za ujenzi wa makazi bora kwa wananchi; na

- g. Uhitaji wa kuendelea kupanga mipango bora kwa ajili ya maeneo ya mijini na vijijini ili kuhakikisha kuwa watu wote wanaishi katika mazingira bora na salama.



**MGAWANYO WA IDADI YA WATU, IDADI YA MAJENGO,
NA IDADI YA HUDUMA ZA KIJAMII KWA MKOA**

Takwimu za Idadi ya Watu na Huduma za Jamii

Katika mwongo mmoja uliopita, idadi ya Watu katika Mkoa wa Dodoma imeongezeka kwa 1,002,037 (Kati ya 2012 na 2022)

Idadi ya Watu 2012
Ilikuwa
2,083,588

Idadi ya Watu 2022
ni
3,085,625




Vituo vya kutolea Huduma za Afya

497




Idadi ya Shule

1,060



Takwimu za Idadi ya Majengo na Anwani za Makazi



Majengo ya Ghorofa
1,461

Majengo ya Kawaida
794,209

Yanayoendelea na
Ujenzi
41,239

ANWANI ZA

MAKAZI

Majengo Yenye
Anwani za Makazi

531,072

Takwimu za Idadi ya Watu na Huduma za Jamii

Katika mwongo mmoja uliopita, idadi ya Watu katika Mkoa wa Arusha imeongezeka kwa 661,945 (Kati ya 2012 na 2022)

Idadi ya
Watu 2012
Ilikuwa
1,694,310

Idadi ya
Watu 2022
ni
2,356,255




**Vituo vya
kutolea
Huduma za
Afyu**

429



**Idadi ya
Shule**


1,102



SENSA YA WATU NA MAKAZI 2022

MKOA WA ARUSHA

Takwimu za Idadi ya Majengo na Anwani za Makazi



Majengo ya Ghorofa
7,180

Majengo ya Kawaida
515,560

Yanayoendelea na
Ujenzi
30,962



Majengo Yenye
Anwani za Makazi

410,498

Takwimu za Idadi ya Watu na Huduma za Jamii

Katika mwongo mmoja uliopita, idadi ya Watu katika Mkoa wa Kilimanjaro imeongezeka kwa 221,847 (Kati ya 2012 na 2022)

Idadi ya
Watu 2012
Ilikuwa
1,640,087

Idadi ya
Watu 2022
ni
1,861,934




Vituo vya
kutolea
Huduma za
Afyu

461




Idadi ya
Shule

1,348



Takwimu za Idadi ya Majengo na Anwani za Makazi



Majengo ya Ghorofa
3,540

Majengo ya
Kawaida
486,916

Yanayoendelea na
Ujenzi
24,635

ANWANI ZA

MAKAZI



Majengo Yenye
Anwani za Makazi

406,838

Takwimu za Idadi ya Watu na Huduma za Jamii

Katika mwongo mmoja uliopita, idadi ya Watu katika Mkoa wa Tanga imeongezeka kwa 570,392 (Kati ya 2012 na 2022)

Idadi ya Watu 2012
Ilikuwa
2,045,205

Idadi ya Watu 2022
ni
2,615,597




Vituo vya kutolea Huduma za Afya

498



Idadi ya Shule


1,381



SENSA YA WATU NA MAKAZI 2022

MKOA WA TANGA

Takwimu za Idadi ya Majengo na Anwani za Makazi



Majengo ya Ghorofa

4,282

Majengo ya
Kawaida

638,604

Yanayoendelea na
Ujenzi

33,511



**Majengo Yenye
Anwani za Makazi**

482,127

Takwimu za Idadi ya Watu na Huduma za Jamii

Katika mwongo mmoja uliopita, idadi ya Watu katika Mkoa wa Morogoro imeongezeka kwa 978,612 (Kati ya 2012 na 2022)

Idadi ya
Watu 2012
Ilikuwa
2,218,492

Idadi ya
Watu 2022
ni
3,197,104



**Vituo
vya Afya**

532



**Idadi ya
Shule**

1,277




51%



49%

**Idadi ya Watu
3,197,104**

Takwimu za Idadi ya Majengo na Anwani za Makazi



Majengo ya Ghorofa

1,331

Majengo ya
Kawaida

724,320

Yanayoendelea na
Ujenzi

36,803

ANWANI ZA

MAKAZI



**Majengo Yenye
Anwani za Makazi**

536,095

Takwimu za Idadi ya Watu na Huduma za Jamii

Katika mwongo mmoja uliopita, idadi ya Watu katika Mkoa wa Pwani imeongezeka kwa 926,279 (Kati ya 2012 na 2022)

Idadi ya
Watu 2012
Ilikuwa
1,098,668

Idadi ya
Watu 2022
ni
2,024,947




**Vituo vya
kutolea
Huduma za
Afya**

444




**Idadi ya
Shule**

932



Takwimu za Idadi ya Majengo na Anwani za Makazi



Majengo ya Ghorofa
1,885

Majengo ya
Kawaida
468,005

Yanayoendelea na
Ujenzi
35,089

ANWANI ZA

MAKAZI



Majengo Yenye
Anwani za Makazi

352,391

Takwimu za Idadi ya Watu na Huduma za Jamii

Katika mwongo mmoja uliopita, idadi ya Watu katika Mkoa wa Dar es Salaam imeongezeka kwa 1,019,187 (Kati ya 2012 na 2022)

Idadi ya Watu 2012
Ilikuwa
4,364,541

Idadi ya Watu 2022
ni
5,383,728




Vituo vya kutolea Huduma za Afya

684




Idadi ya Shule

1,188



Takwimu za Idadi ya Majengo na Anwani za Makazi



Majengo ya Ghorofa
32,219

Majengo ya
Kawaida
827,644

Yanayoendelea na
Ujenzi
53,844



Majengo Yenye
Anwani za Makazi

638,673

Takwimu za Idadi ya Watu na Huduma za Jamii

Katika mwongo mmoja uliopita, idadi ya Watu katika Mkoa wa Lindi imeongezeka kwa 329,376 (Kati ya 2012 na 2022)

Idadi ya Watu 2012
Ilikuwa
864,652

Idadi ya Watu 2022
ni
1,194,028



Vituo vya kutolea Huduma za Afya
303

 **51%**


 **49%**

Idadi ya Watu
1,194,028



Idadi ya Shule
663

Takwimu za Idadi ya Majengo na Anwani za Makazi



Majengo ya Ghorofa
327

Majengo ya
Kawaida
326,065

Yanayoendelea na
Ujenzi
15,006



Majengo Yenye
Anwani za Makazi

275,573

SENSA YA WATU NA MAKAZI 2022


MKOA WA MTWARA

Takwimu za Idadi ya Watu na Huduma za Jamii

Katika mwongo mmoja uliopita, idadi ya Watu katika Mkoa wa Mtwara imeongezeka kwa 364,093 (Kati ya 2012 na 2022)

Idadi ya
Watu 2012
Ilikuwa
1,270,854

Idadi ya
Watu 2022
ni
1,634,947



Idadi ya
Shule

857



Vituo vya
kutolea
Huduma za
Afya

312

Takwimu za Idadi ya Majengo na Anwani za Makazi

ANWANI ZA

MAKAZI

**Majengo Yenye
Anwani za Makazi**

451,095

Majengo ya Ghorofa

507

Majengo ya
Kawaida

488,078

Yanayoendelea na
Ujenzi

22,751

**Majengo
511,336**

SENSA YA WATU NA MAKAZI 2022

MKOA WA RUVUMA

Takwimu za Idadi va Watu na Huduma za Jamii

Katika mwongo mmoja uliopita, idadi ya Watu katika Mkoa wa Ruvuma imeongezeka kwa 471,903 (Kati ya 2012 na 2022)

Idadi ya
Watu 2012
Ilikuwa
1,376,891


Idadi ya
Watu 2022
ni
1,848,794



Vituo vya
kutolea
Huduma za
Afy
382



Idadi ya
Shule
1,046



SENSA YA WATU NA MAKAZI 2022

MKOA WA RUVUMA

Takwimu za Idadi ya Majengo na Anwani za Makazi

Majengo ya Ghorofa

408

Majengo ya
Kawaida

434,989

Yanayoendelea na
Ujenzi

12,931

Majengo
448,328



Majengo Yenye
Anwani za Makazi

370,620

ANWANI ZA

MAKAZI

Takwimu za Idadi ya Watu na Huduma za Jamii

Katika mwongo mmoja uliopita, idadi ya Watu katika Mkoa wa Iringa imeongezeka kwa 251,490 (Kati ya 2012 na 2022)


Idadi ya Watu 2012
Ilikuwa
941,238

Idadi ya Watu 2022
ni
1,192,728



Vituo vya kutolea Huduma za Afya

349



Idadi ya Shule

735

SENSA YA WATU NA MAKAZI 2022

MKOA WA IRINGA

Takwimu za Idadi ya Majengo na Anwani za Makazi



Majengo ya Ghorofa
529

Majengo ya
Kawaida
339,561

Yanayoendelea na
Ujenzi
17,687



Majengo Yenye
Anwani za Makazi

286,161

Takwimu za Idadi ya Watu na Huduma za Jamii

Katika mwongo mmoja uliopita, idadi ya Watu katika Mkoa wa Mbeya imeongezeka kwa 635,206 (Kati ya 2012 na 2022)

Idadi ya
Watu 2012
Ilikuwa
1,708,548

Idadi ya
Watu 2022
ni
2,343,754




Vituo vya
kutolea
Huduma za
Afyā

443



Idadi ya
Shule

1,073



SENSA YA WATU NA MAKAZI 2022

MKOA WA MBEYA

Takwimu za Idadi ya Majengo na Anwani za Makazi



Majengo ya Ghorofa
1,073

Majengo ya
Kawaida
592,896

Yanayoendelea na
Ujenzi
29,085



Majengo Yenye
Anwani za Makazi

466,058

Takwimu za Idadi ya Watu na Huduma za Jamii

Katika mwongo mmoja uliopita, idadi ya Watu katika Mkoa wa Singida imeongezeka kwa 637,421 (Kati ya 2012 na 2022)

Idadi ya
Watu 2012
Ilikuwa
1,370,637

Idadi ya
Watu 2022
ni
2,008,058




Vituo vya
kutolea
Huduma za
Afya

282



Idadi ya
Shule


797



SENSA YA WATU NA MAKAZI 2022

MKOA WA SINGIDA

Takwimu za Idadi ya Majengo na Anwani za Makazi



Majengo ya Ghorofa

290

Majengo ya
Kawaida

440,541

Yanayoendelea na
Ujenzi

22,522

ANWANI ZA

MAKAZI



Majengo Yenye
Anwani za Makazi

332,499

SENSA YA WATU NA MAKAZI 2022


MKOA WA TABORA

Takwimu za Idadi ya Watu na Huduma za Jamii

Katika mwongo mmoja uliopita, idadi ya Watu katika Mkoa wa Tabora imeongezeka kwa 1,100,056 (Kati ya 2012 na 2022)

Idadi ya
Watu 2012
Ilikuwa
2,291,623

Idadi ya
Watu 2022
ni
3,391,679



**Vituo vya
kutolea
Huduma za
Afya**

401



**Idadi ya
Shule**

1,087

Takwimu za Idadi ya Majengo na Anwani za Makazi



Majengo ya Ghorofa

400

Majengo ya
Kawaida

648,178

Yanayoendelea na
Ujenzi

31,525

ANWANI ZA

MAKAZI



Majengo Yenye
